



TAARIFA KWA UMMA

TAMKO LA KULAANI KITENDO CHA UONGOZI WA CHAMA CHA NCCR MAGEUZI KUMTAKA KATIBU MKUU AJIUZULU BILA KUFUATA KATIBA YA CHAMA

Mtandao wa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu (CWHRDs) umepokea kwa masikitiko taarifa ya Bi Martha R. Chiomba, Katibu Mkuu wa Chama cha NCCR MAGEUZI kutakiwa kujiuzulu kwa lazima.

Taarifa tulizozipata kupitia kikao alichokifanya na waandishi wa habari kilichofanyika tarehe 10/5/2022, Katibu Mkuu wa Chama cha NCCR MAGEUZI Bi. Martha Chiomba alieleza kwamba Uongozi wa chama cha NCCR MAGEUZI umemtaka ajiuzulu Cheo hicho kwa madai kuwa hana uwezo stahiki kutumikia Cheo hicho. Katika tamko lake kwa Waandishi wa habari bi Martha amesema vugu vugu la kumuondoa madarakani linafanywa na viongozi wake ikiwa ni sehemu ya mkakati wa Chama cha NCCR MAGEUZI kutaka kuvuna wanachama waliohama chama cha ACT ambao mojawapo ya masharti waliyoyatoa kwa wao kujiunga na NCCR MAGEUZI ni kuwahakikishia watapata nafasi mbali mbali za uongozi ikiwemo ya Ukatibu Mkuu wa Chama.

Bi Martha amesema alijulishwa azma hiyo alipoitwa nyumbani kwa kiongozi mmoja, akiwa na viongozi wengine wawili, ambapo kiongozi huyo alichukua simu ya Bi Martha kwa nguvu , na kwa kutumia kauli ya kibabe kumtaka ajiuzulu na Cheo chake ili ampishe mwanaume. Aidha Bi. Martha Chiomba amesema baada ya kukataa kujiuzulu uongozi wa chama cha NCCR MAGEUZI umekua akitumia watendaji wa chama hicho kumkashifu na kuvuruga amani ya chama. Aidha licha ya Bi Martha kupokea vitisho ikiwemo kazi zake kukataliwa ili aonekana hana uwezo wa kufanya kazi kama sehemu ya kumshinikiza atimize takwa lao la kuachia nafasi ya ukatibu mkuu kwa kujiuzulu mwenyewe.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari Bi Martha amesisitiza kwamba hawezি kufuata agizo la viongozi wake linalomshinikiza kujiuzulu. Aidha amewataka viongozi hao watumie Kanuni, Taratibu na Sheria ikiwemo Katiba ya Chama inayoongoza namna ya kutekeleza azma kama hiyo. Katiba ya Chama cha NCCR MAGEUZI inajinasibu kuwa na nia ya kuwainua wanawake katika ngazi za uongozi na kushiriki katika maamuzi hivyo vitendo kama hivi vya ukandamizaji vinakinzana na dhamira ya chama.

Kufuatia ukandamizaji huu wa haki za wanawake viongozi katika siasa, Mtandao wa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu (CWHRDs) unalaani vikali uongozi wa Chama cha NCCR MAGEUZI kutaka kutumia nguvu kumtoa madarakani Katibu Mkuu wa Chama cha NCCR MAGEUZI kwa sababu ya kutokuwa na uwezo wa kufanya kazi. Mtandao unatahadharisha tabia



na utamaduni wa vyama vingi nya siasa kuleta mivurugano na unyanyasaji wa kijinsia kila chaguzi zinapokaribia bila kujali nguvu nyingi viongozi wanawake wanazotumia kujitolea kuvitumikia na kuviinua vyama husika muda wote nje ya misimu ya chaguzi. Taswira kama hizi zinaleta maswali mengi juu ya ukosefu wa dhamira ya dhati kimatendo ya kuleta usawa wa kijinsia katika uongozi kwa ujumla na hususan baina ya vyama nya siasa, jambo ambalo linawakatisha tamaa wanawake walio katika siasa na kutovutia wanawake wapya, hususan vijana wa kike, kuingia katika ulingo wa siasa.

Tunatoa rai kwa msajili wa vyama nya siasa kuangazia vyama hivi ili kubaini ukiukwaji wa katiba walizojitungia wao wenyewe na kuweka mazingira yatakayotoa ulinzi wa wanawake walio katika siasa ili kulinda haki za wanawake kuchaguliwa au kuchagua viongozi wanaowahitaji. Aidha Mtando unaliomba jeshi la polisi limpe ulinzi anaostahili Bi Martha ili kuepusha walio na nia ovu kuhatarisha usalama wake.

Aidha tunawakumbusha Viongozi wa vyama nya Siasa kufanya kazi kwa ueledi kwa manufaa ya ya wananchi, wakiwemo wanawake, ambao hujinasibu kuwatetea na kukusudia kuwalettea maendeleo pindi wakipata uongozi. Mwisho, kwa kutambua wingi wa idadi yetu wanawake kama wapiga kura nchini, tunatoa wito kwetu sote kuweka nguvu za pamoja kulinda maslahi ya wanawake wenzetu walio na wanaokusudia kuingia katika siasa.

Imetolewa Na:

Mtando wa Wanawake wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania.

Tarehe 11 Mei 2022.